**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI**

**WAKALA YA VYUO VYA MAFUNZO YA MIFUGO - LITA**

**TANGAZO LA KUJIUNGA NA MAFUNZO YA ASTASHAHADA NA STASHAHADA KATIKA MWAKA WA MASOMO 2020/2021**

1. Wakala ya Vyuo vya Mafunzo ya Mifugo (LITA) imeanza kupokea maombi ya kujiunga na mafunzo ya fani za mifugo katika ngazi ya Astashahada na Stashahada katika mwaka wa masomo 2020/2021
2. Mafunzo haya yatatolewa katika Kampasi **nane** za wakala, ambazo ni: Tengeru, Mpwapwa, Morogoro, Buhuri, Madaba, Temeke, Mabuki na Kikulula.
3. Wanafunzi waliomaliza kidato cha nne au cha sita kuanzia mwaka 2010 hadi 2019 wanaotaka kujiunga na mafunzo haya wanakaribishwa kuomba. Aidha, wahitimu wenye vyeti vya Astashahada (NTA Level 5) katika fani zinazohusiana na kozi wanazoomba nao wanaruhisiwa kuomba kujiunga na mafunzo haya katika ngazi ya Stashahada (NTA Level 6 – up grading)
4. Kozi zinazotolewa na Kampasi za Wakala ni kama ifuatavyo :
    - Astashahada ya Afya na Uzalishaji Mifugo *(Certificate in Animal Health and Production - CAHP NTA Level 4 -5*)
    - Stashahada ya Afya na Uzalishaji wa Mifugo *(Diploma in Animal Health and Production – DAHP – NTA Level 4 - 6)*
    - Stashahada ya Afya na Uzalishaji wa Mifugo *(Diploma in Animal Health and Production – DAHP – NTA Level **5 - 6**)*
    - *Stashahada* ya Afya na Uzalishaji wa Mifugo *(Diploma in Animal Health and Production – DAHP – NTA Level 6- upgrading)*
    - Astashahada ya Ufundi Sanifu wa Maabara ya Veterinari *(Certificate in Veterinary Laboratory Technology -CVLT – NTA Level 4-5*)
    - Stashahada ya Ufundi Sanifu wa Maabara ya Veterinari *(Diploma in Veterinary Laboratory Technology – DVLT NTA Level 4- 6)*
    - Stashahada ya Ufundi Sanifu wa Maabara ya Veterinari *(Diploma in Veterinary Laboratory Technology – DVLT NTA Level 6)*
    - Stashahada ya Uendelezaji wa Nyanda za Malisho na Udhibiti wa Ndorobo *(Diploma in Range Management and Tsetse Control-DRMTC)*
      (*NTA Level 6*)

**NB**: *Stashahada* ya Afya na Uzalishaji wa Mifugo *(Diploma in Animal Health and Production – DAHP – NTA Level 6 - upgrading) na* Stashahada ya Ufundi Sanifu wa Maabara ya Veterinari *(Diploma in Veterinary Laboratory Technology – DVLT NTA Level 6- upgrading)* inawahusu wale waliomaliza NTA Level 4 & 5 ambao wanataka kumalizia ngazi ya NTA Level 6.

5. Mawasiliano ya Kampasi zinazotoa mafunzo hayo ni kama ifuatavyo:

| NA | KAMPASI | ANUANI | SIMU | KOZI ZITOLEWAZO |
|---|---|---|---|---|
| **1.** | TENGERU | S.L.P 3101 Arusha | 0734293406 au 0734293407 | DAHP & CAHP (Bweni na Kutwa) |
| **2.** | MPWAPWA | S.L.P 51 Mpwapwa | 0659727926 au 0762422070 | DAHP & CAHP(Bweni na Kutwa) |
| **3.** | MOROGORO | S.L.P 603 Morogoro | 0786203825 au 0754670644 | DAHP & CAHP (Bweni na Kutwa) |
| **4.** | BUHURI | S.L.P 1483 Tanga | 0753799293 au 0713677469 | DAHP CAHP (Bweni na Kutwa) |
| **5.** | MADABA | S.L.P 568 Songea | 0764573807 au 0759343121 | DAHP & CAHP(Bweni na Kutwa) |
| **6.** | TEMEKE | S.L.P 39866 DSM | 0716995351 au 0768098723 | CVLT & DVLT (Kutwa na Bweni) |
| **7.** | MABUKI | S.L.P 115 Misungwi | 0712946724 au 0652397160 | CAHP (Bweni na Kutwa) |
| **8.** | KIKULULA | S.L.P 472 Karagwe | 0684101377 au 0762249190 | CAHP (Bweni) |
| **9.** | LITA HQ | S.L.P 9152 DSM | 0763320080 | |

### 6. Sifa za mwombaji

i. Stashahada ya Afya na Uzalishaji wa Mifugo *(Diploma in Animal Health and Production DAHP –* ***NTA Level 5 - 6****)*

Muombaji awe amehitimu Astashahada ya Afya na Uzalishaji Mifugo (Certificate in Animal Health and Production (AHPC – Term system), au Astashahada ya Kilimo na Uzalishaji Mifugo (Certificate in Agriculture and Livestock Production (CALP) au awe amehitimu Basic Certificate in General Agriculture.

ii. Stashahada ya Afya na Uzalishaji wa Mifugo *(Diploma in Animal Health and Production DAHP – **NTA Level 4 - 6**)*

Muombaji awe amemaliza elimu ya Kidato cha Nne **au** Sita na kufaulu masomo mawili ya Sayansi kati ya Baiolojia, Kilimo, Kemia, Fizikia (Physics/ Engineering Sciences), Hisabati, na Jiografia. Kiwango cha chini cha ufaulu kitakachomwezesha muombaji kukubaliwa kwa wahitimu wa kidato cha Nne (Form IV) ni **D mbili katika masomo ya Sayansi** na **D mbili** kwenye masomo mengine **isipokuwa ya Elimu ya Dini na upishi**;

Kwa wale waliomaliza kidato cha sita (Form six) mwenye ***subsidiaries mbili*** kwenye masomo ya sayansi atakuwa na nafasi zaidi.

**AU** Awe amesoma na kufaulu kidato cha **Nne** na kujiendeleza katika vyuo vya ufundi VETA vyenye mkondo wa mifugo na kupata NVA Level 3 au Trade Test I.

iii. Stashahada ya Afya na Uzalishaji wa Mifugo *(Diploma in Animal Health and Production DAHP – **NTA Level 6 na** Astashahada ya* Ufundi Sanifu wa Maabara ya Veterinari *(Diploma in Veterinary Laboratory Technology **DVLT NTA Level 6**)*

Muombaji awe amemaliza mafunzo ya Astashahada (*Certificate*) katika fani ya *Animal Health and Production CAHP NTA level 5 au Astashahada ya* Ufundi Sanifu wa Maabara ya Veterinari (Technician Certificate in Veterinary Laboratory Technology NTA Level 5*) sawia*

*iv.* Stashahada ya Ufundi Sanifu wa Maabara ya Veterinari *(Diploma in Veterinary Laboratory Technology DVLT NTA Level 4 -6)* Muombaji *awe amemaliza kidato cha Nne (Form IV) au kidato cha Sita (Form VI) kama **Na. 6 ii. Inavyosomeka***

*v.* Stashahada ya Uendelezaji wa Nyanda za Malisho na Udhibiti wa Ndorobo *(Diploma in Range Management and Tsetse Control-DRMTC)*

Muombaji awe amemaliza mafunzo ya Astashahada (*Certificate*) katika fani ya *Animal Health and Production (CAHP NTA evel 5)*

vi. Astashahada ya Afya na Uzalishaji Mifugo *(Certificate in Animal Health and Production - CAHP NTA Level 4-5*)

Muombaji awe amemaliza Kidato cha Nne na kufaulu masomo **mawili** ya sayansi kati ya Baiolojia, Kilimo, Kemia, Fizikia, Hisabati, na Jiografia. Kiwango cha chini cha ufaulu kitakachomwezesha muombaji kukubaliwa ni cha alama ya **D** kwenye masomo manne, (mawili ya sayansi na mawili kwenye masomo mengine isipokuwa Dini na Upishi.

**AU**

Muombaji awe amesoma na kufaulu masomo ya kidato cha **Nne** na kujiendeleza katika vyuo vya ufundi VETA yenye mkondo wa mifugo na kupata NVA Level 3 au Trade Test I.

7. Utaratibu wa kujaza fomu ya maombi

Mwombaji anaweza kuchukua fomu kutoka kwenye **Kampasi (Chuo)** yoyote iliyoko jirani na mahali alipo **au** kupitia Tovuti ya Wakala (Website): *www.lita.go.tz na kupakua fomu. Fomu ijazwe na hatimaye kurudishwa kwenye Kampasi lengwa (angalia jedwali lhapo juu) au kwa njia ya barua pepe zifuatazo:* lita.hq@lita.go.tz

Pamoja na fomu ya maombi iliyojazwa ambatanisha na ***pay-in-slip*** ya ada ya maombi uliyolipia kwenye akaunti ya Wakala kama ilivyoelekezwa kwenye fomu ya maombi.

**Zingatia**: Maombi yoyote yasiyozingatia maelekezo tajwa katika tangazo hili **hayatashughulikiwa**

**Epuka kutapeliwa** Fomu ya maombi (Application form) **HAIUZWI!**

8. Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe **15/08/2020.**

Majina ya watakaochaguliwa yatatolewa kupitia Website ya Wakala: *www.lita.go.tz* na magazeti ya Habari leo na Mwananchi.

**9. Aidha, Wakala inawatangazia wanachuo wote wa mwaka wa masomo 2019/2020 ambao bado hawajaripoti vyuoni hadi leo baada ya vyuo kufunguliwa kwamba mwisho wa kuripoti vyuoni ni tarehe 28/06/2020. Hakuna mwanachuo atakayepokelewa baada ya tarehe 28/06/2020**

Kwa maelezo zaidi wasiliana na :

Mtendaji Mkuu**,**
Wakala ya Vyuo vya Mafunzo ya Mifugo - LITA,
Veterinari Complex,
131 Barabara ya Nelson Mandela,
S. L. P 9152,
**15487 Dar es Salaam**

Simu Na. +255 22 28633479

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI**

# WAKALA YA VYUO VYA MAFUNZO YA MIFUGO - LITA

Wizara ya Mifugo na Uvuvi kupitia Wakala ya Vyuo vya Mafunzo ya Mifugo nchini **(LITA)** imeandaa mafunzo ya muda mfupi kwa wafugaji na wajasiliamali katika Sekta ya Mifugo. Mafunzo yatatolewa kwa **siku saba** kwa kila kozi, kuanzia tarehe **21 Septemba** hadi **17 Oktoba, 2020.**

**Mafunzo yanayotolewa ni kama ifuatavyo**

1. Mbinu za ufugaji bora wa Mifugo ya Asili (ng’ombe, mbuzi na kondoo) na unenepeshaji pamoja na magonjwa, sheria mbalimbali
2. Mbinu za ufugaji bora wa ng'ombe wa maziwa
3. Utunzaji nyanda za malisho, uzalishaji, uvunaji, hifadhi na ulishaji; na umuhimu wa maji kwenye malisho
4. Umuhimu wa vikundi/vyama vya ushirika na taratibu za unzishwaji wake
5. Mbinu za ufugaji bora wa kuku wa asili, nyama na mayai
6. Usindikaji wa maziwa, nyama na ngozi
7. Mbinu za ufugaji bora wa nguruwe na sungura
8. Matumizi sahihi ya mapato yatokanayo na raslimali za mifugo
9. Sheria, kanuni na miongozo inayosimamia sekta ya mifugo na sheria mtambuka

Mafunzo yatatolewa katika kampasi za Tengeru, Kikulula, Morogoro, Mpwapwa, Madaba, Mabuki, Temeke na Buhuri.

Gharama kwa kila mshiriki kwa siku **7** ni shilingi **250,000/=** kwa ajili ya malazi, chakula, mafunzo, shajala na ziara fupi.

**Kwa mawasiliano zaidi tumia namba zifuatazo:** +255 0222 863 479; 0754 746 782; 0754 828 688.

**AU tovuti ya Wakala:** www.lita.go.tz / www.mifugouvuvi.go.tz